# ALELUYA BWANA AMEZALIWA

Ladislaus Kombe
Majani Mapana Tanga
1980




**2.** Aleluya Bwana amezaliwa,
Wachungaji wenda kumtazama,
Amelazwa bandani mwa nyama.
Atukuzwe Mungu juu mbinguni.

**3.** Aleluya Bwana amezaliwa,
Mamajusi nao walifika,
Nazo tunu wakamtolea
Atukuzwe Mungu juu mbinguni.

**4.** Aleleuya Bwana amezaliwa,
Mataifa wanashangilia,
Ukombozi wetu watimia,
Atukuzwe Mungu juu mbinguni.

**5.** Aleluya Bwana amezaliwa,
Tumwendee na nyimbo za shangwe,
Tukampe nazo nyoyo zetu,
Mkombozi atukuzwe daima.